Mafunzo Ya Namna Ya Kuwahudamia Watoto Wanaoishi Katika Mazingira Hatarishi

Mradi wa ushirikiano wa ustawi wa jamii kuhusu UKIMWI kwa ajili ya watoto yatima na waishio katika mazingira hatarishi.

Siku ya 1:
Kuwatambua Watoto Wanaoishi Katika Mazingira Hatarishi

Malengo Ya Mafunzo

- Kuelewa matatizo ya kisaikolojia na kijamii ikiwemo utatuzi wake kuhusu watoto yatima na waishio katika mazingira hatarishi ikiwa ni pamoja na ukuaji wao na tathmini ya kisaikolojia na jini gani ya kuwahudumia
- Kupata uelewa wa namna mbalimbali ya kuwahudumia watoto yatima na wanaoishi katika mazingira hatarishi, na walioathirika/walioathiriwa na VVU/UKIMWI na jinsi ya kutumia uelewa huu katika kuwahudumia.

Malengo Ya Mafunzo

- Kutambua jinsi ambavyo UKIMWI huathiri watoto walio katika mazingira hatarishi nchini Tanzania ikiwemo:
- Kupunguza athari kwa watoto na wazazi wao
- kufahamu na kutambua hatua mbalimbali za maambukizi ya VVU na Ukimwi pamoja na athari zake kwa watoto na familia zao.
- Kuelewa namna ya kukabiliana na maradhi nyemelezi pamoja na matumizi ya dawa za kupunguza makali ya virusi vya UKIMWI (ARV's).

Malengo Ya Mafunzo

- Kutambua na kuweza kushughulikia changamoto mbalimbali za kisaikolojia na kijamii zinazohusiana na UKIMWI kwa watoto yatima na wale waishio katika mazingira hatarishi ikiwemo;
  - kupata matunzo kutoka kwa jamii,
  - kutoa ushauri nasaha,
  - Kukabiliana na unyanyapaa,

Malengo Ya Mafunzo

- Kuelewa rasilimali zilizopo na mifumo ya malezi kuanzia ngazi ya kijiji, Wilaya na Taifa kwa ajili ya watoto waishio katika mazingira hatarishi: (kama vile kamati za UKIMWI za Wilaya/Halmashauri na kamati za watoto wanaoishi katika mazingira hatarishi)
- kujenga uwezo wa kupata huduma husika kutoka kwa jamii, na kufanya kesi menejimenti.
- Kuelewa sera za Tanzania na za kimataifa zinazohusiana na UKIMWI/ watoto waishio katika mazingira hatarishi.

Malengo Ya Mafunzo

- Kuelewa masuala ya kimaadili yahusianayo na utoaji wa huduma na mafunzo kwa watoto waishio katika mazingira hatarishi na walioathirika/walioathiriwa na VVU/UKIMWI.
- Kupata uwezo wa kutunza taarifa, kusimamia/kufuatilia huduma na kuelewa mfumo wa utoaji taarifa za VVU/UKIMWI na zinazohusu watoto waishio katika mazingira hatarishi.

Ili kujiita Msaidizi Ustawi Wa Jamii (Para-Social Worker)*

- Kuhitimu mafunzo ya awali ya Para Social Worker (siku 9)
- Kufanyia mazoezi mafunzo uliyopata kwa miezi 6 chini ya msimamizi aliyepasishwa
- Kumaliza mafunzo ya Para Social Worker sehemu ya II.

*Kipimo kinachotumika na wadau wa Mradi wa Ushirikiano wa ustawi wa jamii kuhusu Ukimwi na watoto waishio katika mazingira hatarishi Tanzania, Taasisi ya Ustawi wa Jamii, Dar es salaam

Kuchagua Wilaya Na Washiriki Wa Mafunzo Ya Msaidizi Wa Ustawi Wa Jamii

- Kuchagua Wilaya kwa kushirikiana na Idara ya Ustawi wa Jamii na Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) pamoja na wadau wengine
- Kuendesha mafunzo juu ya huu mradi kwa viongozi wa serikali za mitaa
- Viongozi katika ngazi ya serikali za mitaa kuchagua washiriki wa mafunzo ya Msaidizi Ustawi wa Jamii
- Viongozi wa serikali za mitaa kuchagua wasimamizi wa Wasaidizi wa Ustawi wa Jamii

Kuvunja Ukimya

Tafadhali angalia orodha ifuatayo, na tafuta mtu mwenye sifa zifuatazo Andika jina la mtu huyo katika sehemu inayohusika. Tafuta mtu ambaye……

•Anashughulika na watoto waishio katika mazingira hatarishi. •Anapendelea chakula sawa na unachokipenda wewe •Yupo katika kamati ya watoto waishio katika mazingira hatarishi. •Tarehe yake ya kuzaliwa ni sawa na yako. •Anafanya kazi katika asasi isiyo ya kiserikali ya kuhudumia watoto yatima na waishio katika mazingira hatarishi. •Ana idadi ya watoto sawa na wewe.	•Amefanya kazi anayofanya sasa kwa muda usiopungua miaka 5. •Ana idadi sawa ya ndugu wa kuzaliwa kama wewe. •Hivi karibuni amehamia kwenye makazi mapya •Amesoma kitabu ambacho wewe pia umekisoma hivi karibuni. • Amesafari kutoka mbali kuliko wewe ili aweze kuhudhuria mafunzo haya. •Amefanya kazi na watoto na familia kwa muda mrefu kupita wewe.

Malengo: Siku Ya Kwanza

Mwisho wa kipindi hiki washiriki watakua na uwezo wa:

- Kufafanua dhana muhimu zinazohusu watoto waishio katika mazingira hatarishi
- Kueleza masuala muhimu yahusuyo hali halisi ya watoto waishio katika mazingira hatarishi
- Kuelezea mchakato wa utambuzi wa watoto waishio katika mazingira hatarishi
- Eleza majukumu ya Msaidizi ***Ustawi wa Jamii katika shughuli za kuwahudumia watoto waishio katika mazingira hatarishi katika ngazi ya jamii.***
- Tambua hatua za mchakato wa huduma wa ustawi wa jamii
- Kuelezea namna Wasaidizi Ustawi wa Jamii huwatambua watoto waishio katika mazingira hatarishi

Dhana Muhimu Namwitikio Kwa Watoto Yatima Na Wanaoishi Katika Mazingira Hatarishi

Hali Ya Watoto Waishio Katika Mazingira Hatarishi Tanzania

- Takribani asilimia 10 ya watoto wa Tanzania ni yatima na wanaoishi katika mazingira hatarishi. Nusu yao wanaishi katika mazingira magumu zaidi.
- Takribani watoto milioni mbili, au asilimia 18 ya watoto chini ya miaka 18 Tanzania, ni yatima au wanaishi katika mazingira hatarishi
- Kati ya hao milioni mbili, asilimia 42 ni yatima wa UKIMWI, na wengine ni yatima kwa sababu za umasikini, unyanyasaji na kutumikishwa.
- Asilimia 53 ya hawa watoto wanaishi na babu au bibi, asilimia 30 wanaishi na ndugu, na asilimia 12, wanalelewa na watoto wengine.
- Asilimia 40 ya watoto wa Tanzania wanaishi chini ya, au sambamba na, kipimo cha umasikini wa taifa

Chanzo: **Tanzania HIV/AIDS and Malaria Indicator Survey 2007-2008**

Mtoto Ni Nani?

- Ni mtu yeyote aliye chini ya miaka 18.

Yatima ni nani?

- Ni mtoto aliyefiwa na mzazi mmoja au wazazi wote wawili.

Mtoto Yatima wa jamii ni nani?

- Ni mtoto aliyetelekezwa au aliyepoteza mawasiliano na wazazi wake.

Mazingira Hatarishi

- Ni hali ya kupungua kwa uwezo wa kuhimili matatizo ya ghafla na ya kudumu ya kijamii, kiuchumi, kimazingira na kisiasa.
- Uwezekano wa mtu binafsi, kaya, na jamii kuathirika kiasi cha kuwa masikini kupindukia kutokana na matukio au michakato inayomzunguka.

Mtoto Aliye Katika Mazingira Hatarishi Ni Nani?

Ni mtoto yeyote ambaye anakosa ama anaweza kukosa malezi na ulinzi wa kutosha.

Mambo matatu yanayosababisha watoto kuwa katika mazingira hatarishi:

- Kupungua kwa uwezo wa kukabiliana na majanga
- Kuwa dhaifu, kwa mfano, kielimu, kiustawi, kiusalama, kimichezo na katika ushiriki wa mambo mbalimbali.
- Kukosa huduma za kutosha na malezi.

Mtoto Aliye Katika Mazingira Hatarishi Zaidi Ni Yupi?

Mtoto aliye katika mazingira hatarishi zaidi ni yule anayeishi katika hali ngumu na ambaye uwezo wake wa kukua na kuendelea kimwili na kiakili uko kwenye hatari

Je unaweza kufikiria baadhi ya mifano ya watoto kama hawa?

Mtoto Aliye Katika Mazingira Hatarishi Zaidi Ni Yupi?

Mifano:

- Mtoto aliyenyanyaswa na kutelekezwa
- Mtoto anayeishi katika kituo cha watoto, rumande, shule au makazi ya watoto wenye mahitaji
- Mtoto aliyezaa mapema kwa kuozeshwa au kupata mimba ya utotoni
- Mtoto ambaye ni mtumishi wa ndani au anatumikishwa utotoni
- Mtoto mwenye ulemavu
- Mtoto anayeishi mtaani
- Mtoto aliye kwenye biashara ya ngono
- Mtoto aliyekinzana na sheria

Mifano Ya Watoto Walio Katika Mazingira Hatarishi Zaidi..

- Watoto wanaokimbia nchi zao kwa sababu za vita au majanga
- Mtoto anayelea wazazi wagonjwa kwa muda mrefu
- Mtoto ambaye ni mlezi katika familia yake
- Mtoto yeyote ambaye ametengwa, kunyanyapaliwa au ananyanyaswa

Matatizo Yanayowakabili Watoto Waishio Katika Mazingira Hatarishi Zaidi

- ***Watoto waishio katika mazingira hatarishi zaidi hukabiliana na matatizo mengi yakiwemo:***
  - Kukosekana kwa mahitaji muhimu ya kisaikolojia na kijamii.
  - Kukosekana kwa chakula/kisichotosheleza au lishe duni
  - Kutokupatikana kwa huduma muhimu za jamii (elimu, afya, maji safi na salama, na huduma za maji taka).
  - Kutoshirikishwa katika maamuzi ya mambo yanayohusu maisha yao.
  - Uporaji wa mali za urithi unaofanywa na ndugu, jamaa au walezi.

Matatizo Yanayowakabili Watoto Waishio Katika Mazingira Hatarishi Zaidi

- UKIMWI/VVU umepunguza uwezo wa asili wa malezi katika familia, matunzo na ulinzi kwa watoto yatima na wale waishio katika Mazingira hatarishi.

Mwitikio Wa Serikali

- Uundaji miongozo ya Taifa ya huduma za jamii kwa ajili ya watoto yatima na waishio katika mazingira hatarishi
- Uchambuzi yakinifu wa hali ya watoto yatima, kwa lengo la kubaini ukubwa wa matatizo yanayowakabili.
- Uundaji wa sera ya Taifa ya UKIMWI (Novemba 2001).
- Kuundwa kwa Tume ya Kudhibiti UKIMWI (TACAIDS) kupitia sheria ya Bunge (2001) ili kuongoza sekta mbalimbali kama mwitikio wa kitaifa dhidi ya VVU/UKIMWI chini ya ofisi ya Waziri Mkuu.

Mwitikio Wa Serikali

- Kuongoza mchakato shirikishi wa utambuzi wa watoto walio kwenye mazingira hatarishi pamoja na kaya zinazohitaji msaada.
- Hivi sasa mpango huo umetekelezwa katika Halmashauri 91. Lengo ni kuzifikia Wilaya zote nchini.

Mwitikio Wa Serikali

- Utengenezaji wa miongozo ya mafunzo ya malezi na uwezeshaji wa hakijamii.
- Kutengeneza miongozo ya kusimamia na kuongza ubora
- Kutengeeneza miongozo itakayotumika kuwasaidia walezi wa watoto walio katika mazingira hatarishi
- Mwongozo wa mipango ya programu za VVU/UKIMWI

Mwitikio Wa Serikali

- Kuanzisha mfumo na usimamizi wa taarifa/takwimu.
- Mfumo wa usimamizi wa taarifa/takwimu unatumika kuwabaini watoa huduma kwa watoto waishio katika mazingira hatarishi na idadi ya watoto waishio katika mazingira hatarishi wanaopata msaada na kufuatilia ubora wa huduma zitolewazo kwa watoto.
- Kupitia Mpango wa Kitaifa wa Gharama Nafuu (National Costed Plan of Action) wa kuongeza jitihada za kitaifa wa kuwahudumia watoto yatima na wanaoishi katika mazingira hatarishi.

Huduma Za Ulinzi Kwa Watoto Waishio Katika Mazingira Hatarishi

Jitihada hizi zote za serikali huchangia katika ulinzi wa watoto walio katika mazingira hatarishi.

Je, ni huduma zipi ambazo huchangia katika ulinzi wa watoto walio katika mazingira hatarishi?

Bungua bongo

Huduma Za Ulinzi Kwa Watoto Waishio Katika Mazingira Hatarishi

- Chakula na Lishe
- Makazi na malazi
- Ulinzi dhidi ya unyanyasaji
- Msaada wa kisheria
- Huduma za Kiafya
- Msaada wa kisaikolojia
- Elimu
- Ulinzi wa mali

Majukumu Na Wajibu Wa Wizara Ya Afya Na Ustawi Wa Jamii(Idara Ya Ustawi Wa Jamii)

- Kuratibu mipango na shughuli/huduma zinazohusu watoto yatima na walio katika mazingira hatarishi.
- Kuandaa miongozo, mfumo wa ufuatiliaji, viashiria vya utekelezaji, zana za ukusanyaji takwimu na mfumo wa utoaji taarifa.
- Kuandaa nyenzo na miongozo ya utambuzi unaolenga watoto yatima na waishio katika mazingira hatarishi na kaya.

Majukumu Na Wajibu Wa Wizara Ya Afya Na Ustawi Wa Jamii(Idara Ya Ustawi Wa Jamii)

- Kutoa ushauri wa kitaalamu kwa kamati elekezi ya kitaifa na kamati ya kiufundi kuhusu masuala ya watoto yatima na waishio katika mazingira hatarishi.
- Kuhakikisha mipango na shughuli zinazohusu watoto yatima na wanaoishi katika mazingira hatarishi, inatekelezwa kwa mujibu wa miongozo ya kitaifa.

Majukumu Na Wajibu Wa Wizara Ya Afya Na Ustawi Wa Jamii (Idara Ya Ustawi Wa Jamii)

- Kuandaa na kuwezesha mafunzo ya stadi kuhusu mchakato wa utambuzi wa watoto yatima na walio katika mazingira hatarishi na Kaya kwa wadau wote wanaotekeleza mpango shirikishi wa kijamii wa malezi, matunzo na ulinzi wa watoto hao.
- Kupokea, kuziboresha, kutunza na kusambaza takwimu na taarifa zinazohusu watoto yatima waishio katika mazingira hatarishi kwa wadau wengine.

Hitimisho

- Utekelezaji wa mpango shirikishi wa kuwahudumia watoto yatima na wanaoishi katika mazingira hatarishi umedhihirisha kuwa na manufaa zaidi katika kushughulikia matatizo ya watoto yatima na wale waishio katika mazingira hatarishi .
- Pia, mpango huu unachangia kukuza ufahamu wa jamii, ushiriki wao, na azma ya kuona kuwa wamiliki wa mpango husika.

Hitimisho

•Mpango huo unahakikisha kuwa watoto yatima wengi na wale wanaoishi katika mazingira hatarishi wanafikiwa na wananufaika na huduma.
•Mpango huo unatoa nafasi kwa wanajamii kutambua matatizo yanayoambatana na uyatima au/na kuishi katika mazingira hatarishi, vyanzo vyake na rasilimali zilizopo za kutatua matatizo husika.

Mapitio Ya Mchakato Wa Ustawi Wa Jamii Wa Kuwahudumia Watoto Yatima Na Waishio Katika Mazingira Hatarishi, Walioathirika/Athiriwa Na Virusi Vya UKIMWI.

Mchakato Na Hatua Za Ustawi Wa Jamii Katika Utambuzi/Uratibu Wa Watoto Yatima Na Waishio Katika Mazingira Hatarishi.

1. Kuwafikia na Kuwatambua
2. Kujenga Uhusiano na watoto Yatima na Familia zao
3. Kutathmini Mahitaji na Uwezo Wao
4. Kutengeneza Mpango wa Huduma: Mitandao, Utambuzi na kutoa Rufaa kwenye Vyanzo vingine vya Huduma.

Mchakato Na Hatua Katika Utambuzi/Uratibu Wa Watoto Yatima Na Waishio Katika Mazingira Hatarishi Kwa Sababu Ya Athari Ya VVU.

5. Kutoa Huduma na Misaada Mingine iliyoko ndani ya uwezo wa taasisi yako
   - Kuwasaidia watoto yatima ambao wameathirika /kuathiriwa na Virusi vya UKIMWI na watoto waishio katika Mazingira Hatarishi.
   - Kutoa huduma ya ushauri nasaha kwa watoto yatima na waishio katika Mazingira hatarishi pamoja na familia zao.
   - Kubuni Mifumo Saidizi kwa ajili ya watoto yatima na watoto waishio katika Mazingira hatarishi na familia zao.
6. Kesi Menejimenti inayoendelea, Utetezi na Ufuatiliaji.

Utambuzi Wa Watoto Yatima Na Waishio Katika Mazingira Hatarishi

USULI

- Zaidi ya watoto 160,000 wanaishi na VVU, na watoto zaidi ya milioni moja wamepoteza mzazi mmoja au wote kutokana na maradhi ya UKIMWI nchini Tanzania
- Kuna watoto milioni 13 ambao wamepoteza mzazi mmoja au wote, kutokana na maradhi ya UKIMWI kusini mwa jangwa na Sahara.

Chanzo: AVERT, 2011

USULI

- Tatizo la virusi vya ukimwi (VVU) na UKIMWI vinafanya kazi ya utetezi wa watoto yatima kuwa ngumu zaidi na kuhitaji uharaka zaidi.
- Kwa sababu ya tishio la UKIMWI watoto wakibakwa au kunajisiwa sio tu wanapatwa na matatizo ya ki-saikolojia na kudhurika kimwili lakini pia inahatarisha maisha yao

Kwa Nini Kuwe Na Msisitizo Kuhusu Watoto Yatima Na Watoto Waishio Katika Mazingira Hatarishi?

- Watoto yatima na watoto wishio katika mazingira hatarishi ni kati ya watu waliodhurika zaidi na UKIMWI lakini pia waliosahaulika katika mipango ya kuratibu UKIMWI
- Kuwekeza katika watoto yatima na watoto waishio katika mazingira hatarishi ni kuwekeza katika nguvu ya kesho na akiba ya jamii na taifa
- Utunzaji wa watoto yatima na waishio katika mazingira hatarishi ni nguvu ya kiunganishi katika uitikiaji wa jamii kwa kuweka mikakati ya kupambana na UKIMWI katika jamii.

Mchakato Na Hatua Za Utambuzi

Idara Ya Ustawi Wa Jamii

Utangulizi

Mpango wa utambuzi wa watoto walio katika mazingira hatarishi unalenga katika :

- kuhakikisha jamii zinashiriki kikamilifu katika utambuzi wa watoto
- Kuotoa fursa kwa wanajamii kutambua matatizo mengine na vyanzo vya hayo matatizo,
- Kubaini rasilimali na fursa zilizopo, na
- Kuchochea ushiriki wa jamii katika kuwalea, kwasaidia na kuwalinda watoto waliotambuliwa na kuwasaidia kukabiliana na maradhi ya UKIMWI

HATUA YA I: Kuandaa Wawezeshaji Ngazi Ya Taifa

- ***Hatua hii ililenga kuwajengea uwezo wawazeshaji katika ngazi ya taifa kwenye maeneo yafuatayo:***
- ***Stadi za uwezeshaji ikiwemo:***
  - Stadi shirikishi za uwezeshaji jamii
  - Kuzingatia haki za Binadamu katika kutengeneza mipango
  - Kufanya uchambuzi wa mazingira hatarishi
  - Stadi za uwezeshaji na mawasiliano
  - Kufahamu zana zitumikazo katika utambuzi wa watoto walio katika mazingira hatarishi

HATUA II: Mkutano Wa Uraghibishi Na Uhamasishaji Ngazi Ya Halmashauri

- Kushirikishana taarifa juu ya mchakato wa utambuzi;
- Kushirikishana na viongozi juu ya hali halisi ya watoto waishio katika mazingira hatarishi;
- Kukubaliana juu ya mazingira hatarishi na hali ya watoto waishio katika haya mazingira;
- Kupata ushirikiano kutoka kwa uongozi wa halmashauri na wadau wengine
- Kuwatambua wadau muhimu
- Kutambua timu ya wawezeshaji katika ngazi ya Wilaya

HATUA III: Kuandaa Timu Ya Wawezeshaji Ngazi Ya Wilaya

- Kuhakikisha wawezeshaji katika ngazi ya wilaya wanaweza kufanya uwezeshaji ipasavyo katika ngazi ya kata na kijiji

Hatua Ya 4 Mkutano Katika Ngazi Ya Kata

- Kushirikishana taarifa juu ya mchakato wa utambuzi wa watoto
- Kujadiliana na viongozi wa kata juu ya hali ya watoto yatima na watoto waishio katika mazingira hatarishi
- Kuwatambua wawezeshaji wa ngazi ya kijiji na kuhakikisha wadau wote wanawakilishwa ipasavyo

Hatua Ya 5. Mafunzo Kwa Ajili Ya Wawezeshaji Ngazi Ya Kata Na Kijiiji/Mtaa

- Kuwapa wawezeshaji mbinu za kuendesha midahalo ya kijamii,
- Jinsi ya kuendesha midahalo na kushirikisha makundi yote,
- Jinsi ya kushirikisha watoto na vijana

HATUA VI: Kufanya Mkutano Na Uongozi Wa Kijiji/Mtaa

- Kuwashirikisha malengo ya mpango wa mradi wa kuwahudumkia yatima na watoto waishio katika mazingira hatarsihi
- Kubaini wadau wengine wanaofanya kazi na watoto yatima na waishio katika mazingira hatarishi katika ngazi ya kjiji.
- Kuwashirikisha katika kutengeneza viashiria vya awali vya kutumika katika kufanya utambuzi wa watoto yatima na wale waishio katika mazingira hatarishi ambavyo vinaendana na desturi za eneo husika

Mkutano Wa Wazi Na Wanajamii Katika Kijiji Na Mtaa

- ***Kuwezesha jamii kujipanga na kufanya utambuzi wa watoto walio katika mazingira hatarishi na kushughulikia mahitaji yao na ya walezi wao hususani katika:***
  - Kutambua viashiria vya mazingira hatarishi kwa mtazamo wa jamii inayohusika.
  - Kutumia viashiria kuweza kutambua watoto walio katika mazingira hatarishi katika kijiji au mtaa

Majadiliano Na Wanakijiji Au Mtaa

- Kujadili juu ya maandalizi ya mpango mkakati wa matunzo, ulinzi na msaada kwa watoto yatima na waishio katika mazingira hatarishi katika kijijji(kuwachagua wawakilishi watakaoandaa huo mpango)
- Kuboresha vigezo vinavyotumika kuwatambua yatima na waishio katika mazingira hatarishi kwa kujumuisha tafsiri za jamii husika
- Kufanya utambuzi wa watoto yatima na waishio katika mazingira hatarishi kwa majina yao na ya walezi wao kulingana na vigezo vilivyokubaliwa na jamii

Tathmini Ya Kijiji/Mtaa

- Kubaini rasilimali zilizo katika kijiji/mtaa ambazo zinaweza kutumika katika kuwatunza, kuwasaidia na kuwalinda watoto yatima na waishio katika mazingira hatarishi
- Kubaini mapungufu, fursa na changamotot katika kijiji/ mtaa

Kutembelea Kaya

- Kuhakikisha majina ya watoto waliotambuliwa katika jamii
- Kufanya upembuzi wa uwezo wa kaya zilizo na watoto yatima na walio katika mazingira hatarishi
  - Kupata taarifa juu ya matatizo wanayopata watoto pamoja na walezi wao
  - Mbinu za ustahimilifu za kaya husika
  - Kupata taarifa juu ya rasilimali vitu, kipato na mambo yanayochangia kaya kuwa katika mazingira hatarishi
- Kupata fursa ya kuongea na watoto pamoja na walezi wao

Kutengeneza Mpango Mkakati Wa Kijiji

- Kutengeneza mpango mkakati wa kijiji wa kuwatunza, kuwasaidia na kuwalinda watoto yatima na waishio katika mazingira hatarishi pamoja na walezi wao.

Mkutano Wa Pili Na Wanakijiji/Mtaa

- Kuthibitisha majina ya watoto waliotambuliwa katika kijiji
- Kuthibitisha mpango mkakati uliotengenezwa kwa ajili ya kuwatunza, kuwasaidia na kuwalinda watoto yatima na waishio katika mazingira hatarishi
- Kuhamasisha ushiriki wa wanakijiji katika kuwatunza, kuwasaidia na kuwalinda yatima na wale waishio katika mazingira hatarishi
- Wanajamii kuandaa mkakati wa ufuatiliaji wa hatua zinazochukuliwa kuwasaidia watoto yatima na kuhuisha taarifa mara kwa mara
- Ni katika ngazi hii ambapo kamati ya watoto waishio katika mazingira hatarishi huundwa(Kitovu cha kuwatunza na kuwalinda watoto)

Baraza La Watoto Yatima Na Waishio Katika Mazingira Hatarishi

- Kupendekeza wawakilishi wa watoto yatima na waishio katika mazingira hatarishi katika Kamata ya watoto waishio katika mazingira hatarishi na kwenye baraza la wilaya la watoto walio kwenye mazingira hatarishi
- Kuwajengea wawakilishi hawa uwezo wa kujieleza na kubaini mahitaji yao
- Kuwapa watoto yatima na waishio katika mazingira hatarishi fursa ya kuupitia mchakato mzima wa utambuzi wa watoto yatima na waishio katika mazingira hatirishi, changamoto zake, na masuala ya kuboresha.

Hatua Ya 7:Kutoa Mafunzo Kwa Wajumbe Wa Kamati Ya Watoto Waishio Katika Mazingira Hatarishi

- Kuwajengea wajumbe uwezo katika:
  - Ufuatiliaji na uratibu wa huduma zitolewazo kwa watoto yatima na waishio katika mazingira hatarishi
- Stadi za utawala na usimamizi wa fedha
  - Kuhuisha taarifa za watoto na kuweka kumbukumbu

Nyenzo Za Utambuzi Na Ufuatiliaji Wa Watoto Waishio Katika Mazingita



FORM No. 1 OVC/MVC

INFORMATION ABOUT THE MOST VULNERABLE CHILDREN REPORT (0 – 18 YEARS) YEAR ..... HALF.....

A : BASIC PARTICULARS

Region..... Council ..... Ward..... Village/Street.....

Number of Heads of Households..... Male..... Female .....

Number of Heads of Households living with OVC/MVC..... Male..... Female .....

Number of all children in the village/street..... Male..... Female .....

Number of Most Vulnerable Children in the village/street..... Male..... Female .....

B: CHILD PARTICULARS

S/No.	Name of a Child	Sex (Male = 1, Female = 2)	Year of Birth	Child Group (OVC/MVC)	Reason for Vulnerability [F]					Date of Identification	Date of Exit	Reason of Exit	Nutritional Status(Y/N)	Completion of Primary Education (Yes = 1, No = 2)	Education Status			
					1	2	3	4	5						Is School Open? (Yes/No)	Education Level	Reason for not at School	Level of Drop out
[A]	[B]	[C]	[D]	[E]						[G]	[H]	[I]	[J]	[K]	[L]	[M]	[N]	[O]



Msaidizi Ustawi Wa Jamii Anawezaje Kuwatambua Watoto Waishio Katika Mazingira Hatarishi Kwenye Jamii?

Hatua ya 1 Hakikisha unapata ushirikiano na msaada kutoka kwa viongozi wa kijiji:

- Jitambulishe kwa viongozi wa kijiji
- Kupata ridhaa ya msaidizi kuhudhuria vikao vya viongozi
- Kupata uelewa wa rasilimali zilizopo kwenye kijiji ikiwa ni pamoja na rasilimali rasmi na zisizo rasmi
- Kupata taarifa juu ya hali halisi ya maambukizi ya VVU katika kijiji
- Kubaini mtazamo wa wanakijiji juu ya suala la watoto walio katika mazingira hatarishi na Ukimwi
- Kupima uelewa wa masuala ya haki kwa watoto walio katika mazingira hatarishi

Hatua ya 2: Tengeneza Uhusiano Wa Moja Kwa Moja Na Wadau Wengine Katika Kijiji

- Viongozi wa serikali na kijiji
- Walimu
- Kamati za elimu/shule
- Viongozi wa dini
- Wahudumu wa afya
- Wazazi au walezi walio katika mazingira magumu
- Asasi za Kiraia
- Polisi Jamii
- Kamati ya VVU/UKIMWI
- Timu za ulinzi kwa watoto
- Viongozi wengine katika jamii
- Kamati ya Ukimwi/VVU ya Sekta mbalimbali (VMAC)

Hatua Ya 3: Jenga Mtandao Ndani Ya Jamii Kwa Ajili Ya Utetezi Na Kufanya Utambuzi Wa Yatima Na Waishio Katika Mazingira Hatarishi

- Develop community understanding of the rights of the child Elimisha jamii juu ya haki za mtoto
- Elimisha jamii juu ya VVU/UKIMWI kulingana na tafiti zinavyosema na sio kuendana na imani potofu au hofu.
- Tafuta kuungwa mkono na watu ambao wameathirika au wameathiriwa na VVU
- Toa huduma kwa walio athirika pamoja na ndugu zao
- Himiza ushiriki wa ndugu katika kutoa msaada

Hatua Ya 4: Jenga Mahusiano Ya Moja Kwa Moja Na Watoto Waishio Katika Mazingira Hatarishi Pamoja Na Familia Zao

- Kutembelea majumbani
- Jenga uaminifu kati yako na watoto na familia zao
- Dumisha mawasiliano ya mara kwa mara na wakati wa matatizo
- Watetee kwa viongozi na watoa huduma katika kijiji/eneo husika
- Watetee kwenye mamlaka za elimu
- Watetee kwa watoa huduma za afya

Majumuisho: Utambuzi Wa Watoto Katika Jamii Na Kujenga Mahusiano

Hatua ya 1: Tafuta kuungwa mkono na viongozi wa kijiji/mtaa

Hatua ya 2: Jenga mahusiano ya moja kwa moja na wadau wengine katika kijiji/mtaa

Hatua ya 3: Jenga mtandao katika jamii wa kukuwezesha kuwatetea na kufanya utambuzi wa watoto waishio katika mazingira hatarishi

Hatua ya 4: Jenga mahusiano ya moja kwa moja na watoto pamoja na familia zao kwa kutumia mtandao uliounda kwa ajili ya utambuzi na kujenga mahusiano

Misingi Ya Mpango Wa Huduma Kwa Watoto Yatima Na Waishio Katika Mazingira Hatarishi

- Imarisha uwezo wa familia au walezi wa kuwatunza watoto pamoja na uwezo wao kiuchumi kwa kutumia mbinu shirikishi katika jamii
- Kuza uwezo wa familia na jamii kukabiliana na mahitaji ya aina zote kwa watoto yatima na walio katika mazingira hatarishi pamoja na walezi wao.
- Imarisha ulinzi na matunzo ya watoto yatima na walio katika mazingira hatarishi ndani ya familia zao na kwenye jamii

Misingi..

- Encourage approaches that allow children to remain in communities rather than being institutionalized **Sisitiza njia zinazowezesha watoto kuishi kwenye jamii zao badala ya kulelewa vituoni.**
- Strengthen the protection and care of Most Vulnerable Children within their extended families and communities

Misingi..

- Kuza uhusiano uliopo katika kuzuia uenezi wa VVU na UKIMWI, huduma za majumbani, na huduma kwa watoto yatima na waishio katika mazingira hatarishi
- Lenga watoto waishio katika mazingira hatarishi na sio tu watoto yatima.
- Zingatia uelewa wa mahusiano ya kijinsia katika shughuli zote
- Sisitiza ushiriki wa watoto wa rika zote katika maamuzi yahusuyo maisha yao.
- Unga mkono shule na hakikisha kuwa watoto wanapata elimu

Misingi…

- Kabiliana na unyanyapaa na ubaguzi.
- Sisitiza kujifunza na ubadilishanaji wa taarifa muhimu
- Jenga na imarisha mahusiano na wadau muhimu katika ngazi zote
- Hakikisha kwamba misaada kutoka nje haidhohofishi jitihada za jamii

Kisa Mkasa

Filamu ya Mwakaila

Filamu ya Mwakaila

- Kutambulisha mada
- Kuonyesha filamu: Tumchezee Mwakaila
- Mjadala katika vikundi vidogo
- Kujadili masuala ya msingi katika kundi kubwa

Filamu ya Mwakaila

- ***Maelekezo ya kazi za vikundi vidogo***
  - ***Jadili katika kikundi kidogo:***

A. Unaionaje filamu hii?

B. Je Mwakaila anaweza kufanana na watoto wengine unaofanya nao?

C. Unawezaje kuja kumtambua mtoto huyu na familia pamoja na hali yao ya maisha ili kumsaidia

D. Fanya majumuisho ya mjadala kwa kuzingatia masuala muhimu ya kufanya kazi na waoto waishio katika mazingira magumu